

“

Njia bora zaidi ya kukabiliana na COVID-19 ni kuhakikisha kuwa sote tumejikinga.

- LESHAN



Jina langu ni Leshan. Ninaishi mjini Boise, Idaho, na nilihamia Marekani hivi majuzi kutoka Kenya. Nilipokea chanjo yangu ya kwanza ya COVID-19 mnamo Machi 2021 ilipokuwa ikipeanwa kwa walio chini ya miaka 65. Hivi majuzi nilipewa dozi ya Pfizer ya kuimarisha kinga ya mwili ili kuhakikisha kuwa nimejikinga kikamilifu na pia ninawalinda walio karibu nami dhidi ya COVID-19. Janga lilipoanza, nilikuwa chuoni, mbali na nyumbani na sikuwa na mahali pa kwenda. Hali hii ilifanya mambo kuwa magumu sana kwangu. Hii ilinichochea kupata chanjo punde ilipoanza kutolewa, ili niweze kuwaona wazazi wangu. Nilifurahi kuwa wazazi wangu waliweza kuja Marekani kwa ajili ya sherehe yangu ya kuhitimu iliyofanyika mwezi Mei mwaka jana. Haya yote yaliwezekana kwa sababu ya chanjo. Kupata chanjo kulituwezesha kusherehekeea kuhitimu kwangu na pia kuonana baada ya muda mrefu.

Najua watu wengi hawajaweza kuwaona wapendwa wao kutokana na COVID-19, na ninafahamu kwamba imekuwa ngumu kwa watu wengi kupata chanjo na pia dozi za kuimarisha kinga ya mwili. Nashukuru na ninajihisi mwenye bahati sana kwa kupokea chanjo na dozi ya kuimarisha kinga ya mwili, na pia nawashukuru wazazi wangu kwa kupata chanjo. Nawahimiza watu wote wapate chanjo kwa manufaa ya jamii na wapendwa wao ili tuweze kujumuika pamoja tena. Haswa sasa ambapo kuna virusi vya aina ya Omicron, Nahimiza kila mtu apate chanjo na dozi ya kuimarisha kinga ya mwili. Njia bora zaidi ya kukabiliana na COVID-19 ni kuhakikisha kuwa sote tumejikinga.